



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA BUKOBA
(Barua zote ziadikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. KGR/BDC/S.2/70/20

03/06/2021

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba amepokea Kibali cha Ajira Mbadala kwa barua ya tarehe 20 Mei, 2021 yeye Kumb. Na. FA.170/368/01”B”/61 kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Kwa hiyo, anawatangazia Watanzania wote wenye Sifa na uwezo wa kujaza nafasi **02** kama inavyoonekana hapa chini:

MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU II – (NAFASI 02) – TGS B

SIFA ZA MWOMBAJI

- Awe na elimu ya kidato cha IV au cha VI.
- Awe na cheti cha Astashahada (**Technician Certificate - NTA LEVEL 5**) cha Utunzaji wa Kumbukumbu katika mojawapo ya fani za Afya, Masjala, Mahakama na Ardhi.

MAJUKUMU YA KAZI

- Kutafuta kumbukumbu/nyaraka/mafaili yanayohitajika na wasomaji.
- Kuthibiti upokeaji, uandikishaji wa kumbukumbu/nyaraka.
- Kuchambua, kuorodhesha na kupanga kumbukumbu/nyaraka katika makundi kulingana na somo husika (Classification and Boxing) kwa ajili ya matumizi ya ofisi.
- Kuweka/kupanga kumbukumbu,nyaraka katika reki (file racks/cabinets) katika masjala/vyumba vya kuhifadhia kumbukumbu.
- Kuweka kumbukumbu (barua, nyaraka nk) katika mafaili.

Sanduku la Posta 491 Bukoba, Kagera **Simu:**

028 2220287, **nukushi:** 028 2221839 **barua pepe:** ded@bukobadc.go.tz, **tovuti:** bukobadc.go.tz

